

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA KILINDONI (“KILINDONI WSSA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

#### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W 18-025

Mnamo tarehe 17 Novemba 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Kilindoni (Kilindoni WSSA) la kutaka kurekebisha bei za huduma za majisafi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Jedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

#### Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Kiwango cha Matumizi	Bei ya sasa	Bei Zinazopendekezwa					
			2018/19	Badiliko (%)	2019/20	Badiliko (%)	2020/21	Badiliko (%)
Majumbani	1-5	300	367	1,400	7	1,500	7	1,600
	5-10		383	1,450	10	1,600	6	1,700
	10-30		400	1,500	13	1,700	6	1,800
	≥30		433	1,600	19	1,900	5	2,000
	1-10	335	348	1,500	13	1,700	6	1,800
	11-30		363	1,550	16	1,800	6	1,900
Taasisi	≥30		378	1,600	31	2,100	5	2,200
Biashara	1-10	390	285	1,500	13	1,700	6	1,800
	11-30		297	1,550	16	1,800	6	1,900
	≥30		310	1,600	31	2,100	5	2,200
Magati	1	1,000	50	1,500	13	1,700	12	1,900

**Jedwali 2: Bei za maji za sasa na zinazopendekezwa kwa wateja wasio na Dira  
(Shilingi/Mwezi)**

Kundi la wateja	Bei ya sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2018/19	Badiliko (%)	2019/20	Badiliko (%)	2020/21	Badiliko (%)	2021/22
Majumbani	5,500	173	15,000	20	18,000	11	20,000
Taasisi	11,500 – 80,000	73.9 - 87.5	20,000 - 150,000	13.3 - 23	25,000 - 170,000	17.6 - 20	30,000 - 200,000
Biashara	11,500 – 13,500	73.9 - 85.2	20,000 - 25,000	20.0 - 25	25,000 - 30,000	20.0-33.3	30,000 - 40,000

**Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya  
(Shilingi kwa maunganisho mapya)**

Kundi la wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2018/19	Badiliko (%)	2019/20	Badiliko (%)	2020/21	Badiliko (%)	2021/22
Majumbani	22,500	33	30,000	33	40,000	25	50,000
Taasisi	22,500	122	50,000	20	60,000	17	70,000
Biashara	22,500	122	50,000	20	60,000	17	70,000

Kwa mujibu wa wasilisho la Kilindoni WSSA, bei, ada na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ya kutosha kumudu gharama halisi za uendeshaji. Mamlaka ya maji Kilindoni imebainisha kuwa mabadiliko ya bei na tozo yanayopendekezwa yataiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji zilizoongezeka sana ukilinganisha na mwaka 2011 ilipoanza kutumia bei ya sasa.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 23 Mei 2019, katika Ukumbi Magereza Kilindoni – Mafia** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe **30 Mei 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA Kanda ya Mashariki, **GHOROFA YA SABA, JENGO LA LAPF, MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, S.L.P 72175 DAR ES SALAAM** au Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kilindoni zilizopo mjini Kilindoni.

**Imetolewa na: Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)  
6 Mei 2019**